

MKATABA WA KUPANGA NYUMBA

KATI YA

AWAZI JUMA MSOMI

NA

YAKET INTERNATIONAL LTD.

10 NOVEMBER, 2023

MKATABA WA KUPANGA NYUMBA

MKATABA huu umetengenezwa leo tarehe 10. ya Mwezi wa 11., 2023 kati ya **Bwana AWAZI JUMA MSOMI** wa S.L.P Pwani Mkuranga (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **Mwenyenyumba**) kwa upande mmoja;

NA

Yaket International Ltd. wa S. L. P. 105722, Pwani, Mkuranga (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **Mpangaji**) kwa upande mwingine.

KWA KUWA:

- A. Mwenyenyumba ni mmiliki halali wa nyumba iliyopo Mkuranga, Pwani (itakayojulikana katika mkataba huu kama “Nyumba”)
- B. Mpangaji kwa hiari yake mwenyewe akiwa na akili timamu amekubali kupanga nyumba hiyo kwa matumizi ya ofisi ya kampuni.
- C. **HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:**

1. Gharama ya nyumba kwa mwaka ni shilingi Milioni Moja na laki Nane (1,800,000) ambazo zitalipwa kwa awamu mbili, ambapo leo tarehe ya kusainiwa kwa mkataba huu 10. ya mwezi wa 11. 2023, atalipa shilingi laki tisa tu (900,000) yakiwa ni malipo awamu ya kwanza. Halafu kiasi kinachobaki yaani shilingi laki tisa tu (900,000) atalipa wakati anakabadhiwa nyumba tarehe 15. ya mwezi 11. 2023.
2. Mkataba huu ni wa kipindi cha mwaka moja tu yaani kuanzia tarehe 10. mwezi wa 11. 2023 mpaka tarehe 10. mwezi wa 11. 2024
3. **Mwenyenyumba** atamkabidhi nyumba Mpangaji mara baada ya malipo kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 1 hapo juu.
4. Mpangaji atawajibika kulipa kodi ya umeme na maji kwa kipindi chote cha upangishaji
5. Mpangaji anakiri kutobadilisha kitu chochote alichokikuta kwenye nyumba bila ridhaa ya mwenyenyumba
6. Thamani zote za nyumba zitakabidhiwa kama mpangaji alivyokabidhiwa awali

7. Mkataba huu unaweza kuvunjika kusitishwa kwa mpangaji atakaye kiuka masharti yafuatayo;
 - 7.1 Kushindwa kulipa pesa husika iliyobaki kabla ya kukabidhiwa ufunguo wa nyumba.
 - 7.2 Haparuhusiwi kuingizwa kilevi cha aina yoyote ndani ya nyumba.
 - 7.3 Kutenda jambo ambalo kimaadili halifai.
 - 7.4 Hairuhusiwi kupangisha/kukaa na mtu mwingine bila ridhaa ya mwenyenyumba.

Imetiwa saini na **Bwana Awazi Juma Msomi** ambaye ninamfahamu leo/ ametambulishwa kwangu na **JAMALI**....., leo
Tarehe.....10.....mwezi.....11..... 2023

M. Juma
.....
MWENYE NYUMBA

SHAHIDI:
Jina: *Ditrick Gray*
Sahihi: *Gray*
Cheo: *Kwaki*
Tarehe:.....10.....mwezi.....11.....2023



Imetiwa saini na Meneja wa kampuni kwa niaba ya mpangaji ambaye ni **Yaket International co. Ltd.** Ambaye ninamfahamu/ ambaye ametambulishwa kwangu na **JAMALI**..... leo
Tarehe.....10.....mwezi.....11..... 2023.



T. B. M.
.....
MPANGAJI

SHAHIDI:
Jina: *Ditrick Gray*
Sahihi: *Gray*
Cheo: *Kwaki*
Tarehe:.....10.....mwezi.....11.....2023

